

# SAYANSI YA MICHEZO



## KUCHEZA HUWASAIDIA WATOTO KUKABILIANA NA MAFADHAIKO NA WASIWASI KATIKA MAISHA. PIA HUNUFAISHA AFYA YA MWILI NA AKILI

WAKATI BORA NA MUAFAKA WA MTOTO KUJIFUNZA KUPITIA MCHEZO NI AKIWA MCHANGA. SAYANSI INAONYESHA UCHEZAJI UNAWEZA KULETA MABORESHO MAKUBWA NA KUSAIDIA UKUAJI WA UBONGO.

URAFIKI UNAJENGWA NA KUKUZWA KWA KUPITIA MICHEZO. HII NI MUHIMU KWA AJILI INASAIDIA UWEZO WA KUJIDHIBITI NA UJUZI WA KIJAMII.

KUCHEZA PIA HUWASAIDIA WATOTO KUWA MAKINI: UTAFITI UNAONYESHA KUWA WATOTO HUWA MAKINI ZAIDI NA KAZI ZAO ZA SHULE BAADA YA MAPUMZIKO NA MICHEZO.

KUCHEZA HUKUZA UBUNIFU, HUPUNGUZA MSONGO WA MAWAZO NA HUBORESHA USINGIZI.

KUCHOCHEA UBUNIFU WA WATOTO (KUPITIA MICHEZO YA MANENO, MASHAIRI AU KUSIMULIA HADITHI) KUNAKUZA UKUAJI WA LUGHA NA UJUZI WA KUSOMA NA KUANDIKA.

KATI YA UMRI WA MIAKA MIWILI (2) HADI SABA (7), MICHEZO YA KUIGIZA KATI YA WATOTO HUWASAIDIA KUWAIMARISHA KIMAWAZO.

TAFITI ZINAONYESHA KWAMBA KUCHEZA KUNAWEZA KUSAIDIA KUBORESHA UFANISI WA MATIBABU YA UGONJWA WA ADHD (UGONJWA WA UPUNGUFU WA MAKINI NA KUHANGAIKA), HASA IKIHUSIANA NA MAFANIKIO YA KIJAMII.

SAYANSI INATHIBITISHA KWAMBA KUCHEZA HUSAIDIA KUUNDA MAHUSIANO KATI YA MZAZI NA MTOTO WAKE. WAZAZI HUWA WASIKIVU KWA WATOTO WAO WACHANGA WAKATI WA MCHEZO, NA MZAZI ANAPOKUWA MSIKIVU ZAIDI, MTOTO MCHANGA HUWA MAKINI ZAIDI.

WATOTO AMBAO HAWASIKILIZWI KIHISIA, HAWAVUMILIWI NA AMBAO WANAPITIA MAGUMU HUWA NA UWEZEKANO MKUBWA WA KUWA NA MSONGO WA MAWAZO, AMBAO UNAHUSISHWA NA MATATIZO YA AFYA YA AKILI, MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA NA UCHANGAMFU KWA KIASI KIDOGO..



UNODC
United Nations Office on Drugs and Crime

Kwa taarifa zaidi, tembelea:
**www.unodc.org/listenfirst**

PAKUA **APP** YA
HURU

**Kwa hisani ya watu wa Ufaransa**